**Noa bongo, jenga maisha yako**

**"Kabumbu barani Afrika-si mchezo wa miguu pekee"**

**EPISODE SEVEN: "Funga mabao, Usimzabe vibao"**

**MWANDISHI: Chrispin Mwakideu**

**WAHARIRI: Andrea Schmidt, Thelma Mwadzaya**

**Orodha ya wahusika / KIPINDI CHA SABA:**

- MSIMULIZI

**SCENE ONE: AT AUNT LILY'S**

- Safina (Mke,13)
- Metogba (mume, 28)
- shangazi Lily (mke, 33)

**SCENE TWO: A PHONE CALL**

- Jonathan (mume,15)
- Komora (mume,14)
- Mhe. Makemba. (mume, 55)

**SCENE THREE: POLICE STATION IN TAMBARARE CITY**

- Chedede (mume,14)
- Safina (mke,13)
- Metogba (mume,28)
- shangazi Lily (mke, 33)
- Inspekta Tino (mume, 40)

**SCENE FOUR: AT MAKEMBA'S HOME**

- Mhe. Makemba. (mume,55)
- Jonathan (mume,15)

**SCENE FIVE: SOCCER CLINIC AT THE CITY STADIUM**

- Mchanganyiko wa sauti za wavulana na wasichana (13+)
- Metogba (mume, 28)
- Wakasa (mwenyekiti wa uongozi wa mpira, mume, 54)
- Inspekta Tino (mume, 40)
- Raisi (mume, 67)

**INTRO:**

**1. NARRATOR:**

Hamjamboni na karibuni tena kwa kipindi hiki ambacho waweza kunoa bongo, ili ujenge maisha yako, hiki ni kipindi chetu cha saba katika hadithi hii ya mchezo wa mpira wa miguu kwa jina" **"Kabumbu barani Afrika".** Katika makala yaliyopita, Chedede – alishangaa alipokamatwa na askari kwa tuhuma za kulivamia duka la Shah Elevtronics alipokuwa mazoezini. Rafiki yake, Safina alifufukuzwa nyumbani na shangazi yake, naye mcheza soka Metogba aliirai jamii kuwapa wavulana na wasichana nafasi yakuyaimarisha maisha vilevile kushiriki katika kiliniki yake ya soka. Je, jawabu la ombi lake litakuwa nini? Je, Dede atapatikana na hatia?. Haya na mengine mengi ni katika kipindi hiki cha leo kwa jina **"Funga mabao, usimzabe vibao".** Kwanza kabisa shangazi Lily ana mgeni...

**SCENE ONE: AT AUNT LILY'S**

2. **SFX: KNOCKING ON DOOR**

3. **SHANGAZI LILY:** Naam, ni nani?

4. **METOGBA: (from outside)** Ahm, ni mimi Metogba. Tafadhali naomba kuongea na wewe....

5. **SHANGAZI LILY:** Metogba? Samahani... sikufahamu na sina tabia ya kuzungumza na watu nisiowajua...

6. **METOGBA:** Nimekuelewa, lakini ni kuhusu mpwa wako, Safina.

**Silence, short pause**

7. **SFX: LOCKS AND BOLTS BEING OPENED.**

8. **SHANGAZI LILY: (Worried voice)** Yuko salama? Tafadhali nieleze kilichomsibu…....

9. **METOGBA:** Usiwe na hofu, yu salama salimini. **(Calls out)** Safina!, hebu panda ngazi uje.

10. **SFX: STEPS CLIMBING STAIRS...**

11. **SAFINA: (Timidly)** Shikamoo shangazi Lily..

12. **METOGBA:** Safina amenieleza yote yaliyotokea. Samahani, mimi ni mkufunzi wake wa soka. Niko hapa kwa niaba yake kukuomba umregeshe nyumbani na umruhusu aendelee kucheza kabumbu. Msichana huyu ana kipaji.

13. **SHANGAZI LILY:** Safina, Nilikasirishwa kwa vile hukunisikiliza, lakini ulinitia wasiwasi sana**.** Ikiwa haya ninayoelezwa ni ya kweli, basi nakuunga mkono. Karibu tena nyumbani!

14. **METOGBA:** Unaona Safina, nilikwambia, ukijua tu kujieleza, mambo huwa shwari. Hilo ni tatizo moja tumetatua. Sasa nataka niijue hatma ya Chedede ...

15. **SHANGAZI LILY: (surprised)** Chedede? Amekumbwa na yapi tena?

16. **SAFINA:** Alikamatwa na askari tulipokuwa mazoezini leo. Anashukiwa

alivunja duka la Shah electronics. Lakini nilimueleza Metogba kuwa haiwezi kuwa kweli kwa sababu nilikuwa naye hapa tulipokusaidia ulipokuwa.... aa... **(hesitates)** unakumbuka?

**17. METOGBA:** Namuamini. Nimemfahamu Chedede kwa muda mfupi na sidhani kama anaweza kufanya kitendo kama hicho...

**18. SHANGAZI LILY: (Thinking aloud)** Maskini mtoto wa watu... lazima tumsaidie. Twendeni!

**19. NARRATOR:** Wakati hao watatu walipokuwa wakijiandaa kuelekea kwenye kituo cha polisi alikozuiliwa Chedede, nyumbani kwa Makemba Jonathan alibarizi sebuleni akisikiliza muziki mororo wakati simu ilipoita...

**SCENE TWO: A PHONE CALL**

**20. SFX: MUSIC IN THE BACKGROUND, TELEPHONE RINGS**

**21. VOICE MAIL/MHE. MAKEMBA:** Umefika nyumbani kwa mheshimiwa Makemba, mbunge wako, tafadhali acha jina na nambari yako baada ya mlio na nitakupigia baadaye. Asante.

**22. SFX: BEEP THAT COMES BEFORE A VOICEMAIL MESSAGE**

**23. KOMORA: (Talking in a drunken voice)** Mhe. Makemba, ni mimi Komora. Sina nambari ya simu kwa sasa lakini ntaipata karibuni, (kicheko) kazi imekamilika. Chedede alikamatwa hii leo. Bado niko na runinga zilizokuwa dukani. Nieleze tutakutana lini na wapi unipe pesa zangu zilizosalia. Wewe ni kiboko yao!

(kicheko) kwa heri...

**24. SFX: PUBLIC TELEPHONE RECEIVER BEING PLACED BACK. VOICEMAIL MACHINE BEEPS**

**25. JONATHAN: (Utterly shocked)** La... hapana... Haiwezekani! Babangu!? na Komora!? Haiwezekani!

**26. NARRATOR**: Taarifa hizo kuwa babake alihusika katika njama ya kumtuhumu rafikiye Chedede zilimshtua Jonathan. Hakuyaamini aliyoyasikia... Jee, atakuwa na ujasiri wa kumsuta babake? Kwa upande mwengine, katika kituo cha polisi...

**<u>SCENE THREE: AT THE TAMBARARE POLICE STATION</u>**

**27. SFX: OFFICES SOUND (PHONES RINGING, COMPUTER WORKING ETC)**

**28. SHANGAZI LILY:** Habari Inspekta, tumekuja kumuona kijana mmoja. Jina lake ni Dede... Chedede. Alikuwa...

**29. INSPEKTA TINO:** Munataka kumuona yule mwizi wa runinga? Nifuateni.

**30. SFX: STEPS OF SEVERAL PERSONS, OFFICE SOUNDS FADING OUT, BUNCH OF KEYS. METAL DOOR BEING OPENED**

**31. CHEDEDE:** Safina! Metogba, na shangazi Lily... nimefurahi kuwaona.

**32. INSPEKTA TINO:** Muna dakika tano...

33. **CHEDEDE:** Sikuiba, nina apa mbele ya Mungu. Sio mimi...

34. **METOGBA:** Twajua vyema si wewe Chedede, lakini lazima tuwe na ushahidi.

35. **SHANGAZI LILY: (Breaks down into tears)** Nakuhurumia... pole sana... hustahili haya.

36. **SAFINA:** Shangazi... tafadhali usilie.

37. **SHANGAZI LILY:** Nyinyi hamuelewi...

38. **METOGBA:** Chedede, Wewe ni mmoja wa wanasoka hodari katika timu yetu na kutakua na pengo kubwa ikiwa hutorudi.

39. **INSPEKTA TINO: : (Shouts)** Muda wenu kwisha!

40. **SHANGAZI LILY:** Si ulisema tuna dakika tano.

41. **INSPEKTA TINO:** Ndio, lakini hapa ndani kwa mahabusu muda huo ni dakika mbili na nusu...

42. **SFX: METAL DOOR BEING LOCKED**

43. **NARRATOR:** Chedede alijawa na masuali mengi baada ya Shangazi Lily kumtembelea. Kipi kilichokuwa kinamliza? Kweli alimuonea huruma kiasi hicho? Au kulikua na mengine? Wakati Dede akiyatafakari hayo, Jonathan alikuwa anamsubiri babake arudi nyumbani.

**SCENE FOUR: MAKEMBA’S RESIDENCE**

**44. MHE. MAKEMBA:** Habari, Jonathan. Mazoezi ya kabumbu yanaendeleaje?

**45. JONATHAN: (Coldly)** Vyema. Una ujumbe kwenye simu!

**46. MHE. MAKEMBA:** Mbona una simanzi? Changamka kijana wangu.

**47. JONATHAN: (Still cold)** Naweza kukabiliana na hali yoyote isipokuwa yale nilioyasikia...

**48. MHE. MAKEMBA:** Aaaah…taratibu. Ni nani aliyepiga simu?

**49. SFX: PUSHES BUTTON TO PLAY THE VOICEMAIL MESSAGE BY KOMORA.**

**50. NARRATOR:** Ni vigumu kuukanusha ukweli haswa ukiwa bayana kama katika hali iliyomkuta Mhe. Makemba. Je, Jonathan ni jasiri atakayeweza kutetea haki hata ikiwa sifa ya babake itaingia doa? Asubuhi iliyofuatia katika kiliniki ya soka, Metogba hakuwa tayari kukabiliana na yatakayosibu.

**SCENE FIVE: SOCCER CLINIC AT TAMBARARE CITY STADIUM**

**51. SFX: MIXED VOICES OF MANY BOYS AND GIRLS VERY LOUD**

**52. METOGBA:** Kimya!... kila mtu anyamaze!

**53. SFX: WHISTLE BLOW... SILENCE**

**54. METOGBA:** Sawa! Kwa hakika sikutarajia kuona vijana wengi namna hii. Ni bayana kuwa ombi langu lilisikika... sasa, kwanza nitahitaji niwagawanye makundi tofauti. Kisha tutaanza mazoezi.

**55. SFX: POLICE SIRENS... FOLLOWED BY MOTORCYLES AND CARS**

**56. METOGBA:** Lahaula!... Bwana Wakasa, kwani kucheza kandanda ni uhalifu katika nchi hii?

**57. WAKASA: (Terrified)** Hawa sio polisi tu pekee, Metogba. Msafara huu ni wa raisi wa nchi yetu! Timizeni wanavyotaka kwa usalama wenu.

**58. SFX: MOTORCYCLES AND CARS STOPPING, CAR DOORS BEING OPENED AND SHUT, MURMURS OF CHILDREN**

**59. INSPEKTA TINO: (Shouting)** Kila mmoja arudi nyuma! Ndio, nyote rudini nyuma. Raisi anataka kuwahutubia wananchi akiwa hapa kwenye kliniki hii ya soka.

**60. SFX: MURMURS AND FAINT CHEERS FROM CROWD.**

**61. RAISI:** Wananchi wenzangu, nimezisikia taarifa njema kuwa mamia ya watoto wadogo waliokuwa wakishiriki kwenye uasi dhidi ya serikali yangu wameachiwa huru.Baadhi yao wao wako hapa katika mafunzo haya ya mpira. Naipongeza serikali yangu kwa juhudi hizi.Hatua hii inalinufaisha taifa letu kwa sababu badala ya mapambano ya risasi, watapambana kufunga magoli .

**62. SFX: FAINT CHEERS AND APPLAUSE AGAIN.**

**63. RAISI:** Serikali yangu itafanya kila iwezalo kuiimarisha sekta ya michezo. Tumeweka nadhari ya kuwa wenyeji wa kinyang'anyiro kijacho cha soka barani Afrika na itatimia! Tutajenga barabara mpya, viwanja vipya, tena vya kisasa kama vilivyoko barani Ulaya na vijana watapata ajira.Kwahiyo, nachukua fursa hii kukifungua rasmi kitengo hiki cha mazoezi na mafunzo ya kandanda. Shukran.

**64. SFX: HUGE APPLAUSE**

**OUTRO:**

**65 : NARRATOR:** Makofi hayo ya waliokusanyika kwenye uwanja wa michezo ndiyo yanayotuhitimishia kipindi chetu cha saba cha, **"Soka barani Afrika"**. Jonathan ana mipango gani? Je, Chedede atashtakiwa au atapelekwa jela baridi? Metogba atafanya nini baada ya raisi kuchukua wajibu wa usimamizi wa kiliniki yake bila kumueleza? Kwa haya na mengine mengi yatakujia katika kipindi kijacho. Ukitaka kusikiliza kipindi hiki tena au kipindi chochole kilichopita, tazama kurasa za tovuti zetu katika **www.dw world.de/**lbe. Hadi wakati mwengine, kwaherini!